

# HALMASHAURI YA MJI KASULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: +255282810335

Tovuti: [www.kasulutc.go.tz](http://www.kasulutc.go.tz)

Barua pepe: [td@kasulutc.go.tz](mailto:td@kasulutc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji  
Halmashauri ya Mji Kasulu  
S. L. P 475  
KASULU.

19/08/2022

## TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kasulu anapenda kuwataarifu waombaji walioomba kazi za Kada za Mtendaji wa Mtaa III, Katibu Mahsusi III, Dereva II na Mtunza Kumbukumbu Msaidizi II, kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe **29 Agosti, 2022 hadi tarehe 04 Septemba, 2022.**

Wasailiwa walioitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

- i. Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwaajili ya utambuzi
- ii. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na kitambulisho cha NIDA, kitambulisho cha mpiga kura, kitambulisho cha mkazi, hati ya kusafiria, leseni ya udereva na barua ya utambulisho toka serikali ya Kijiji/Mtaa
- iii. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **VYETI VYAO HALISI** kuanzia cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, VI na vyeti vya taaluma/ utaalumu, na leseni ya udereva (Kwa wasailiwa kada ya udereva)
- iv. Kila msailiwa atajigharamia chakula, usafiri na malazi
- v. Kila msailiwa azingatie tarehe, muda na mahali alipopangiwa kufanyia usaili
- vi. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa mamlaka husika (**kama TCU, NACTE au NECTA**)
- vii. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia masharti ya tangazo husika.

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI  
KASULU

**RATIBA YA USAILI KUANZIA 29/8 – 4/9/2022**

<b>Na</b>	<b>Kada</b>	<b>Tarehe ya Usaili wa Mchujo</b>	<b>Tarehe ya Usaili wa Vitendo</b>	<b>Tarehe ya usaili wa mahojiano ya ana kwa ana</b>	<b>Mahali Usaili utakapofanyika na Muda</b>
1	Dereva II	29/08/2022	30/08/2022	31/08/2022	Chuo cha ualimu Kabanga kilichopo Mbondo –kibondo road Saa 2:00 Asubuhi.
2	Katibu Mahsusi III	Hakuna	30/08/2022	31/08/2022	Chuo cha ualimu Kabanga kilichopo Mbondo –kibondo road Saa 2:00 Asubuhi.
3	Mtendaji wa Mtaa III	01/09/2022	Hakuna	02-04/09/2022	Chuo cha ualimu Kabanga kilichopo Mbondo –kibondo road Saa 2:00 Asubuhi.
4	Mtunza Kumbukumbu Msaidizi II	Hakuna	Hakuna	02/09/2022	Chuo cha ualimu Kabanga kilichopo Mbondo –kibondo road Saa 2:00 Asubuhi.

Imetolewa na,



Pascalina A. Mabena

**Kny;MKURUGENZI WA MJI**

**HALMASHAURI YA MJI KASULU**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI  
KASULU